JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA

SIMU MKURUGENZI : **225 028 501375**
OFISI ZOTE**: 40334**
FAX: **255 028 500785**

S.L.P. 1333
MWANZA.

20.04.2017

T A N G A Z O

ZABUNI YA UTOAJI WA HUDUMA YA USAFI, UKUSANYAJI NA USAFIRISHAJI WA TAKA NGUMU – ENEO LA KATI YA JIJI

KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/02.

1. Halmashauri ya Jiji la Mwanza inapenda kuwaalika watu binafsi, makampuni, Ushirika, Taasisi au vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria wenye nia, uwezo na uzoefu wa kufanya kazi hiyo kutuma maombi yao kwa zabuni hii katika vyanzo mbalimbali vya mapato kama ifuatavyo:-

Na.	Maelezo *[orodha ya kina, ya maelezo ya mahitaji/viwango na vipimo]*	*FUNGU YA KUTOLEA ZABUNI*
1.	**KATA YA PAMBA**	**ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/02./01**
2.	**KATA YA NYAMAGANA**	**ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/02./02**
3.	**KATA YA ISAMILO**	**ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/02./03**
4.	**KATA YA MIRONGO**	**ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/02./04**
5.	**KATA YA MBUGANI**	**ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/02./05**
6.	**KATA YA MABATINI**	**ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/02./06**
7.	**KATA YA IGOGO**	**ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/02./07**
8.	**STENDI YA NYEGEZI**	**ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/02./08**

2. Maombi yote ya zabuni yazingatie masharti yafuatayo
3. Ada ya maombi ya zabuni ni shilingi laki moja tu **(100,000/=)** ambazo hazitarejeshwa. Mzabuni atatakiwa kuambatanisha nakala halisi ya risiti ya ada ya maombi. Ada hii ni kwa maombi ya kila Kata kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali namba 1.
   i. Wakati wa kuwasilisha maombi mwombaji awasilishe vitu vifuatavyo:-
      a) Nakala ya leseni .
      b) kivuli cha VAT.
      c) Nakala ya usajili wa TIN (kwa Kampuni).
      d) Nakala halisi ya hati ya usajili wa kampuni. (Company registration certificate)
4. Kampuni itakayoomba zabuni hii ni lazima iambatanishe orodha kamili ya viongozi pamoja na wasifu wao (Curriculum Vitae).Viongozi wawe ni wale watakaosimamia moja kwa moja utekelezaji wa zabuni hii.
5. Kampuni itakayoomba zabuni hii ni lazima iwe na vitendea kazi bora na vya kisasa kwa ajili ya kufagia, kukusanyia taka ngumu, kuwakinga watumishi na ajali/ madhara mbalimbali pamoja na vyombo vya kusafirishia taka ngumu kutoka kwenye maeneo ya kaya, biashara, stendi, masoko na

maeneo ya wazi na kuzipeleka kwenye vituo vya kukusanyia taka ngumu (collection points) zilizoidhinishwa kutumika na Halmashauri ya Jiji la Mwanza.

6. Kampuni itakayoomba zabuni hii ni lazima iambatanishe wasifu wake (Organizational Profile) inayoonyesha uzoefu wa utoaji wa huduma ya usafi na uzoaji wa taka ngumu kwenye majiji na manispaa mbalimbali zilizoko nchini.
7. Kampuni itakayoomba zabuni hii ni lazima iambatanishe **TAMKO RASMI DHIDI YA VITENDO VYA RUSHWA** iliyosainiwa na mwombaji mwenyewe.
8. Kampuni itakayoomba zabuni hii ni lazima iwe na wataalam wenye uzoefu wa kutosha na waliohitimu katika fani za Usimamizi wa Mazingira (Environmental Management), Afya ya Mazingira (Environmental health), Uhandisi wa Mazingira (Environmental engineering/Sanitary engineering). Wataalam hao wasiwe watumishi wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza. Nakala halisi ya vyeti vya Shahada vya wataalam vilivyothibitishwa viambatanishwe ndani ya maombi ya zabuni.
9. Waombaji watatakiwa kuambatanisha "Bank Statement" ya miezi kumi na miwili (12) Dhamana ya zabuni: Dhamana ya zabuni (Bid Security) italetwa kwa njia ya Banker's Cheque ambayo itakuwa ni asilimia mbili (2%) ya marejesho ya miezi mitatu ya kiasi alichoahidi mzabuni.
10. Mwombaji wa zabuni endapo atachaguliwa atahitajika kuleta dhamana ya kufanya kazi (Performance Bond), kwa njia ya Banker`s cheque kutoka banki husika yenye thamani ya malipo ya miezi mitatu ya kiasi alichoahidi kuilipa Halmashauri.(Hi ni kwa wazabuni watakao shinda zabuni hii).
11. Mwombaji awasilishe zabuni Original na nakala mbili (2) endapo maelezo ya original na nakala yatatofautiana Original ndio itatumika kwenye tathmini.
12. Zabuni ijazwe vizuri, iwekwe kwenye bahasha isiyo na maandishi yoyote (Plain) na juu ya bahasha iandikwe, namba ya zabuni, kazi inayoombwa, Original & Copy, Anuani ya mkurugenzi bila kuwekwa alama yoyote.
13. Mwombaji atakayeshindwa masharti haya atakuwa amejiondoa mwenyewe kwenye mchakato mzima wa zabuni.
14. Uongozi haulazimiki kuchagua zabuni yoyote.
15. Mwisho wa kupokea zabuni ni **saa nne (4)** kamili asubuhi (saa ya Afrika Mashariki) ya tarehe **12/05/2017** siku ya **Ijumaa** katika **ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji zilizopo Halmashauri ya Jiji la Mwanza.** Waombaji au wawakilishi wa waombaji wanaalikwa kushuhudia ufunguzi. Ufunguzi utafanywa mara tu baada ya saa ya mwisho ya kupokea zabuni mbele ya waombaji au wawakilishi wa waombaji waliochagua kuhudhuria ufunguzi huo utakaofanyika katika Ukumbi Mkubwa katika ofisi za Halmashauri ya Jiji la Mwanza.
16. Zabuni zitawasilishwa kwa Mkurugenzi Mkuu wa halmashauri ya Jiji la Mwanza.

    Anuani ya kutuma zabuni hizo ni:-

    MKURUGENZI
    HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA
    S.L.P. 1333, **MWANZA**
17. Zabuni ambazo zitachelewa kwa muda uliopangwa na zabuni zitakazotumwa kwa mtandao (e-mail) hazitapokelewa.

KIOMONI KIBURWA KIBAMBA
MKURUGENZI WA JIJI
MWANZA.